JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI
**BARAZA LA VETERINARI TANZANIA**

# TANGAZO KUHUSU WADAIWA WA "RETENTION FEES" YA KILA MWAKA KWA MADAKTARI WA MIFUGO NA WATAALAMU WA MIFUGO WASAIDIZI WALIOSAJILIWA NA BARAZA

Baraza la Veterinari Tanzania limeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 3 cha Sheria ya Veterinari (Sura 319) ili kusimamia taaluma ya veterinari na huduma za afya ya mifugo nchini.

Baraza la Veterinari Tanzania linawatangazia Madaktari wa Mifugo na Wataalamu wa Mifugo Wasaidizi kuhuisha usajili wao wa kila mwaka kwa kulipa "Retention Fees" kulingana na vifungu vya 23(1) na 37(1) mtawalia vya Sheria ya Veterinari (SURA 319).

Hivyo, Madaktari wa Mifugo na Wataalam wa Mifugo wasaidizi waliosajiliwa na wanaodaiwa wanatakiwa kulipia "Retention Fees" na malimbikizo yote kabla ya tarehe 15/04/2023 ili kuepuka hatua zitakazochukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Veterinari (SURA 319).

Orodha ya Madaktari wa Mifugo na Wataalam wa Mifugo Wasaidizi na hali ya ulipaji wa "Retention Fees" kwa kila mwaka inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. **www.mifugouvuvi.go.tz**

**Imetolewa na:**

**MSAJILI**
**BARAZA LA VETERINARI TANZANIA**

CamScanner

Alisema licha ya kukithiri kwa vitendo hivyo, Waislamu wanajivunia uwapo wa

kee Tanzania na Afrika Mashariki ambaye anafanya kazi hiyo.

# Ulega: Tunaboresha sera ya mifugo ilete mchango

**Na Jenifer Gilla**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema wizara ipo katika hatua ya mwisho ya kuboresha sera ya mifugo ya mwaka 2006, ili ilete mchango chanya katika maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo juzi kupitia mtandao wa 'Club house' wakati akichangia mada ya mwelekeo na mageuzi katika sekta hiyo na kuongeza kuwa wizara imejipanga kuhakikisha kuwa mifugo na uvuvi vinateka soko la kimataifa.

Ulega alisema maboresho hayo ni moja ya mikakati ya wizara hiyo ya kuleta mageuzi katika sekta za mifugo na uvuvi na kwa sasa wataalam wanamalizia kuipitia ili ipelekwe katika mchakato wa kisheria kwa ajili ya kupitishwa na kuanza kazi.Alisema mkakati mwingine ni kuhamasisha na kufuatilia utoaji wa chanjo kwa kufuata utaratibu maalum kwa mujibu wa Sheria ya Ugonjwa wa Mifugo namba 17 ya Mwaka 2003 ili kuboresha na kutunza mifugo hiyo na kufikia viwango vya kuuza kimataifa.

Aidha, wana mpango wa kuboresha upatikanaji wa majani na maji ili kuhakikisha mifugo haifariki kwa kukosa malisho na kuondoa migogoro inayoendelea kati ya wakulima na wafugaji kutokana na mifugo kuvamia mashamba kunakosababishwa na uhaba wa chakula.

Kuhusu uvuvi, Ulega alisema mwaka wa fedha 2022/2023 serikali ilitoa Sh. bilioni 20 kati ya hizo Sh. bilioni 17.5 zilitolewa kwa ajili ya kuboresha ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika Ziwa Victoria, lengo likiwa ni kukuza ubora wa bidhaa hiyo ili ikubalike sokoni.

Alisema lengo la wizara ni kukuza soko la mifugo ndani na nje ya nchi ikiwamo kuuza nyama nje ya nchi, huku Watanzania wakila nyama za kutosha ili kuwaepusha na magonjwa yanayosababishwa na ukosefu wa protini ikiwamo udumavu.

"Tumeshafika hatua ya kuuza tani 12,000 mpaka 14,000 ambapo tumetoka katika kuuza tani 1,700, lakini tunaona kuna nafasi ya kuuza zaidi duniani katika masoko mbalimbali," alisema Ulega.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA NYAMAGANA**
**SHAURI LA MIRATHI NO.26/2023**

**YEKUNO S/O AMLAK CHITEJI ..... . MSIMAMIZI**
**DHIDI YA**
**FRANK MATHEW CHITEJI.... . . . MAREHEMU**

**KWA: YEYOTE ANAYEHUSIKA**
**KUITWA SHAURINI**

Mwombaji mtajwa hapo juu amefungua shauri la mirathi katika mahakama hii, hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.
Yeyote anaehusika anatakiwa kuhudhuria mahakama tarehe 17.04.2023 saa 2.00 asubuhi yeye binafsi au wakili wake.
Zingatia kwamba kutokuhudhuria kwenu kwa tarehe tajwa, kesi hii itaendelea kusikilizwa bila ninyi kuwepo mahakamani.
Imetolea kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 16/03/2023.

J.A.Mpuya
**HAKIMU MKAZI MKUU**
**MAHAKAMA YA WILAYA NYAMAGANA**
**MWANZA**
PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE
MWANZA



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya MISSENYI**
**Kituo cha KANYIGO**
**Mkoa KAGERA**
**Usimamizi wa mirathi Na 03/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU NESTORY YAKOBO wa KIGARAMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA DIOCLES RUTAKUBANGULA IZOBA**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wnaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 19 mwezi 04 mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo

**Zingatia**
Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 29 mwezi 03 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO


CamScanner

# Machinjio ya kisasa PSSSF yauza nyama nje

**Na Joseph Mwendapole,**
MOROGORO

KIWANDA cha nyama cha Nguru Hills Ranch, Morogoro chenye machinjio ya kimataifa, kimeanza kusafirisha nyama nje ya nchi na kimepata soko kubwa nchi za Uarabuni.

Kiwanda hicho kinamilikiwa kwa ubia na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) yenye asilimia 39 ya hisa, Eclipse ya nchini Oman yenye asilimia 46 na busara yenye asilimia 15.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa kiwanda hicho, Erick Cormack, wakati wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF), walipotembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki.

Alisema ranchi yao iliyoko Wilaya ya Mvomero, Wilaya ya Morogoro ina uwezo wa kuhifadhi ng'ombe 10,000 na mbuzi 15,000 kwa wakati mmoja.

Alisema machinjio ina uwezo wa kuchinja ng'ombe 100 na mbuzi 1,000 kwa siku na asilimia 80 ya nyama inayozalishwa kwenye machinjio hiyo inasafirishwa nje ya nchi na asilimia 20 inauzwa kwenye soko la ndani.

Alisema soko kubwa la nyama ya machinjio yao ni Qatar, Oman Bahrain, United Arab Emirates (UAE), Kuwait, Saudi Arabia, Malasyia, Indonesia na China.

"Nyama yetu inakidhi viwango vya kimataifa kwasababu tumeshaanza kuuza kwenye masoko hayo kwa wingi kuanzia mwaka jana imepokewa vizuri na inaweza kushindana na nyama inayotoka kwenye nchi mbalimbali duniani," alisema.

Alisema wamesajili watu waliozunguka nchi nzima kwaajili ya kununua ng'ombe wa kunenepeshwa kwenye ranchi hiyo kabla ya kuchinjwa.

Alisema, ng'ombe akishafikishwa kwenye ranchi hiyo anakaa miezi mitatu akinenepeshwa kwa virutubisho mbalimbali na baada ya hapo akikidhi vigezo ndipo huchinjwa.

Miradi mingine ambayo PSSSF inaifanya kwa ubia ni Kiwanda cha Chai cha Mponde Tea Tanga, Karanga International Leather Industries Limited kilichopo Moshi, Kilimanjaro na Mamba Miamba Ginger kilichoko Same mkoani Kilimanjaro.

CamScanner



UHURU UK 3.

# Ulega anadi sekta ya uvuvi kimataifa

**Na MWANDISHI MAALUMU,** *Italia*

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewahimiza wawekezaji kutoka nchi za nje kuja kuwekeza katika sekta ya uvuvi kwa kuwa imekuwa ikipata mafanikio makubwa.

Pia, amesema sekta ya uvuvi ina fursa kubwa katika uwekezaji kutokana na uwepo wa uendelevu wa uvunaji wa rasilimali za uvuvi zinazoongeza usalama wa chakula na kuondoa umaskini.

Waziri Ulega alitoa wito huo wakati wa kikao cha kufunga Maadhimisho ya Mwaka wa Kimataifa wa Uvuvi Mdogo na Ukuzaji Viumbe Maji (International Year of Artisanal Fisheries and Aquaculture-IYAFA 2022) kilichofanyika jijini Roma, nchini Italia.

Akizungumza katika kikao hicho, Ulega alisema kuna fursa nyingi zilizopo katika sekta ya uvuvu ikiwemo kuendelea kuboresha mnyororo wa thamani wa uvuvi hususan zao la dagaa ambalo linavuliwa kwa wingi Tanzania na kuhusisha jamii kubwa ya wavuvi hususan wanawake.

Alisema wadau wa kikao hicho wanapaswa kuendeleza usimamizi wa rasilimali ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji na sekta ya uvuvi iendelee kuleta tija.

Katika kikao hicho, Waziri Ulega alitoa ombi la Tanzania kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa wadau wanaojihusisha na uvuvi mdogo (SSF Summit 2024) kutokana na uwepo wa rasilimali nyingi za uvuvi nchini.

Alitumia fursa hiyo kuelezea mafanikio makubwa ambayo Tanzania imeyapata katika kutekeleza mwongozo wa kuwainua wavuvi wanaojihusisha na uvuvi mdogo.

Miongoni mwa mafanikio hayo ni Kuzindua Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kutekeleza Mwongozo wa Uvuvi Mdogo (NPoA-SSF Guidelines) huku akiongeza Tanzania imeshirikisha uzoefu wake katika utekelezaji wa mpango huo kwa baadhi ya nchi zikiwemo Malawi, Ethiopia na Shelisheli.

Pia, Tanzania imeanzisha jukwaa la wanawake wanaojihusisha na uvuvi (TAWFA) na dawati la jinsia katika sekta ya uvuvi, hatua ambayo inakwenda sanjari na dhamira ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, ya kuwainua wanawake nchini.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula (FAO), Dk. QU Dongyu, alimshukuru Ulega kwa kukubali mwaliko huo huku akiahidi shirika lake litaendelea kuipa kipaumbele Tanzania katika kutekeleza miradi ya maendeleo na wataendelea kushirikiana katika kuboresha sekta ya uvuvi.

Waziri Ulega alialikwa kushiriki katika maadhimisho hayo kutokana na Tanzania kufanya vizuri katika utekelezaji wa Mradi wa Uvuvi Mdogo, ambapo ilikuwa nchi ya kwanza duniani kuzindua mpango kazi wa kitaifa wa kutekeleza mwongozo wa uvuvi mdogo.

jumla wa hivi sasa wa mfuko kuwa na

Hata hivyo, alisema tayari kuna

unamilikiwa na wabia watatu.

## MAZUNGUMZO

UHURU UK 5.




**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kimataifa la Kilimo na Chakula (FAO), Dk. Qu Dongyu, Ofisi za Makao Makuu ya Shirika hilo, Jijini Roma, Italia mwishoni mwa wiki. (Na Mpigapicha Maalumu).**

n Jenista Mhagama as Minister of State in the Prime Minister's Office (Policy, Parliament and Co-
am yesterday. Photo: State House

government to fight the deterioration of moral values.
Gracing this year's Quran

and workforce, he told the gathering, urging that parents all over the

role to play here, he

TURN TO Page2

THE GUARDIAN Page 1.

# Minister primes sector for 2024 global fisheries meet

By Guardian Reporter

FISHING stakeholders have been urged to be prepared as Tanzania readies to host the small-scale fisheries (SSF) summit next year.

Abdallah Ulega (pictured), the Livestock and Fisheries minister, issued this appeal in remarks at the closing session of the international year of artisanal fisheries and aquaculture (IYAFA) 2022 meeting in the Italian capital of Rome at the weekend.

Explaining achievements attained in implementing SSF guidelines to boost small scale fishermen, he pointed at the launching of the national task force for the management of small-scale fishing plan.

Tanzania has collaborated with Malawi, Ethiopia and Seychelles, exchanging experience in implementing the guidelines, he stated, citing the Tanzania Women Fishing Association (TAWFA) and the gender desk for the fishing sector within the ministry.



These measures are in line with efforts by President Samia Suluhu Hassan to enhance women income generating activities, he said, while Dr Qu Donguy, the United Nations Food and Agriculture Organisation (FAO) director general thanked the minister for accepting the invitation.

He said that the FAO gives priority to Tanzania's efforts in implementing various development projects, especially in boosting the fishing sector.

The minister had a special role in the meeting as FAO sees the country's performance in implementing the SSF guidelines as salutary, being the first country in the world to launch the guidelines for small fishermen, the director noted.

Urged foreign investors to take up opportunities in the fishing sector, he said there are openings in the value chain for sustainable harvesting of fish for the local market and export.

He pointed at sardines as an ample resource where plenty of fishing practitioners are involved, including women, urging stakeholders at the meeting to focus on sustainable management of fishing resources and in aquaculture development.

CamScanner